JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA SABA

JULAI 2023




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.


www.pmo.go.tz



# Waziri Mhagama atembelea Mnara wa Shujaa AHAMAD MZEE

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama ametembelea Mnara wa Shujaa UD 5826 L/CPL AHAMAD MZEE katika kata ya Kitaya Halmashauri ya wilaya ya Nanyamba Mkoani Mtwara.

Waziri ametembelea mnara huo Nanyamba Mkoani Mtwara siku chache kuelekea siku ya Mashujaa ya kitaifa inayotarajiwa kufanyika tarehe 25/08/2023 katika Uwanja wa Mashujaa uliopo Mji wa serikali Mtumba Jijijni Dodoma.

Shujaa Ahmad Mzee alikuwa Muajiriwa wa Jeshi la Wananchi alipokuwa akitekeleza majukumu yake ya kikazi akiwa na umri wa Miaka 21 alipelekwa Mpakani mwa kijiji cha Kitaya akiwa na jukumu la Ulinzi wa Taifa la Tanzania katika nafasi ya Mpiga mzinga wa kuangusha ndege.

Katika kutekeleza Majukumu yake tarehe 14 April 1972 wakati ndege za Mreno zikitokea Msumbiji Helicopter na Jet Fighters zilipiga mabomu kijiji cha Kitaya na katika Mapambano hayo Shujaa Ahmad Mzee aliangusha Jet Fighter mbili, moja ilianguka ardhi ya Tanzania Mto Ruvuma na Nyingine ilianguka ardhi ya Msumbiji.

Kwenye Mapambano hayo Shujaa Ahamad Mzee alijeruhiwa baada ya Kupigwa na fighter na alichukuliwa na kukimbizwa Mtwara Ligula Hospitali na huko ndiko alikofia.

.



# Waziri Mhagama - Kampeni ya Kili Challenge 2023 kusaidia utekelezaji wa Afua za UKIMWI

Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya Virusi Vya UKIMWI ambapo mwaka huu mpya wa fedha wa 2023/2024 zimetengwa fedha nyingi zaidi kuhakikisha kila Wizara na Taasisi ya Umma zinawezeshwa katika mapambano hayo.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama Mjini Moshi mkoani Kilimanjaro mara baada ya kuwapoke Mashujaa waliojitolea kupanda Mlima Kilimanjaro na wengine wengine kuuzunguka kwa baiskeli ili kuchangisha fedha kwa ajili ya kuchangia juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

“Serikali iliweka Lengo A (objective A) ambalo kila Wizara na Taasisi ya Umma zinatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya masuala ya VVU na UKIMWI. Katika mwaka 2022/23, Serikali ilitenga shilingi bilioni 41 na mwaka 2023/24 imeweka fedha zaidi," alieleza

Aidha, licha ya fedha zilizo katika Lengo A, katika mwaka 2022/23, TACAIDS ilitengewa shilingi bilioni 14.98 kwa ajili ya masuala ya VVU na UKIMWI pekee na mwaka 2023/24 zimetengwa shilingi bilioni 25.86 ikiwa na lengo la kuendeleza mapambano hayo. Pamoja na hilo TACAIDS imeendelea kuufikia umma wa Watanzania kupitia program mbalimbali ikiwemo mafunzo na kutoa miongozo juu ya mapambano haya.

"Tumeendelea kutoa miongozo ya kudhibiti VVU na UKIMWI pamoja na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa ili kuhakikisha jamii inapata elimu kuhusu masuala haya na kupinga unyanyapaa" Amekaririwa Mhe Mhagama.

Amesema kuwa, ili kuzifikia SIFURI TATU kutokuwa na Maambukizi Mapya, Kutokuwa na Unyanyapaa na Ubaguzi, na Kutokuwa na Vifo Vitokanavyo na UKIMWI, ambapo amesema ipo haja ya kuendelea kuunga mkono jitihada hizo kupitia Kuchangia Mfuko wa Kili Challenge ili kuwa na matokeo yanayotarajiwa.

Kwenye Kampeni ya Killi Challenge jumla ya shilingi milioni 543 ziligawiwa kwa Halmashauri zinazohudumia Konga nchini ili kuwasaidia katika shughuli zao.

Waziri Mhagama ameushukuru uongozi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) pamoja na wadau mbalimbali katika kuandaa na kuwezesha Kampeni ya Kilimanjaro Challenge against HIV and AIDS" kufanyika kila mwaka na kutambua jitihada zinazofanywa na Uongozi wa Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Geita bila kusahau Sekretarieti za Wilaya za Hai na Moshi kwa kuratibu na kuwa wenyeji wa tukio hilo kila mwaka.

Aidha aliwapongeza mashujaa walioshiriki katika kampeni hiyo na kutoa rai kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi mwaka ujao katika Kampeni ya Kili Challenge.




# SERIKALI Yatoa msaada wa kibinadamu, Nanyamba na Tandahimba

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) imetoa misaada ya kibinadamu kwa kaya 184 za kata ya Kitaya Halmashauri ya wilaya ya Nanyamba na kaya 160 kwa kata ya Michenjele Halmashauri ya wilaya ya Tandahimba.

Zoezi hilo limeongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu) Mhe, Jenista Mhagama Mkoani Mtwara amesema kwa kutumia sheria no 6 iliyotungwa mwaka 2022 ya usimamizi wa maafa, kazi yetu ni kufanya tathimini na kutoa Mkono wa pole kwenye Majanga yanayohusu binadamu mahali popote.

"Nitoe wito kila yanapotokea majanga na maafa, kwanza liwe jukumu letu kufarijiana kwa karibu; na kutoa taarifa za dalili za majanga yanapotokea, na kuangalia ni mambo gani ya msingi yafanyike ili kurudisha hali katika utaratibu wa kawaida" alihimiza.

Waziri Mhagama amesema, tumepokea tathimini iliyowakilishwa ikionesha madhara yaliyojitokeza kwa wananchi katika eneo hili katika maeneo kadha kwa kadha katika makazi, chakula,na nyenzo za kufanyia shughuli za kiuchumi

Amefafanua kwamba Serikali imekuja kutoa Mkono ili tuweze kushirikiana na nyie katika kujibadilishia hali katika kipindi hiki chote, "nikweli Serikali imeendelea kuwa na nyie kwa nguvu kubwa na ya ziada zaidi," alisema Mhe. Waziri

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassani kwa kutushika Mkono wananchi yanapotokea majanga ya kibindamu, yanapotokea mafuriko, na vinapotokea vimbunga, tunajisikia faraja.

Tumepokea magodoro 190 tumepokea ndoo kubwa 380, na ndoo kubwa za lita ishirini 190, tumepokea blanketi za watoto 190 na blanketi za watu wazima 380 na mikeka 380 na mabati 5700 na kaya zinazostahiki ni 184 zilizoordheshwa kwa sasa katika Halmashauri ya wilaya ya Nanyamba.

Kanali Ahmedi ameongeza kusema Halmashauri ya wilaya ya Tandahimba Ilipokea vifaa vya msaada wa kibinadamu kwa waathirika 160, tuna mabati 4800 kuna magodoro 160, mikeka 320 na mablanketi 320, ndoo kubwa za lita ishirini 320 na tayari zimeundwa kamati mbalimbali kwa ajili ya kuhakiki

Naye Mbunge wa Nanyamba Mhe. Abdallah Chikota amesema Tunashukuru kwa msaada wa kibinadamu na kipekee nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa sababu asiyeshukuru kwa moja hata kumi hawezi kushukuru.



# TAASISI Zinazotekeleza programu ya kuendeleza kilimo na uvuvi (AFDP) zatakiwa kufanya kazi kwa malengo

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulika na maswala ya Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama amezitaka taasisi zinazotekeleza Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) kufanya kazi kwa malengo na kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi ambao umewekwa katika programu hiyo.

Kauli hiyo ameitoa alipokuwa katika ziara ya kikazi ya kutembelea Shirika la Uvuvi la Nchini (TAFICO) Jijini Dar es Salaam, ambapo alisema (TAFICO) ni Moja ya taasisi za Serikali iliyopewa majukumu katika programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi, yenye lengo kubwa la kuongeza tija na faida katika mazao yatokanayo na Kilimo na uvuvi ikiwa ni pamoja na ukuzaji wa mazao yatokanayo na viumbe maji kupitia teknolojia ya kisasa.

Akizitaja Wizara na Tasisi zinazotekeleza Programu hizo chini ya Uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kuwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, (TAFICO) na (ZAFICO)

Waziri Mhagama alitaka Taasisi hizo kuzingatia ubora, na thamani ya fedha katika mradi mzima "Natarajia kila senti itakayowekezwa katika mradi huu itaenda kujibu na kuleta matokeo halisi tena yakiwa chanya na yatakayosaidia nchi yetu kusonga mbele na kupata maendeleo endelevu kwa wananchi na Taifa kwa Ujumla, Alisisita."

Akizungumza katika Ziara hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi alisema, Serikali Imeweka mkazo katika kuhakikisha kwamba Nchi inanufaika na Rasilimali maji hasa katika eneo la uvuvi, kupitia mradi wa (AFDP) hivyo "Sisi kama watendaji tupo tayari kuweka msisitizo na kuhahakisha kwamba haya yote yanakamilika kwa wakati na kuleta Tija kwa Taifa letu." Alisisitiza Dkt. Yonazi

Kwa Upande wake Afisa Mtendaji mkuu wa Shirika hilo Bw. Dennis Simba alisema kuwa, (TAFICO) imejipanga na ipo tayari katika kuhakikisha kwamba inafungua njia ya kwenda katika uvuvi wa Bahari Kuu na mnyororo mzima wa thamani, na kuongeza kuwa miradi kumi na moja (11) iliopo katika programu hii itatekelezwa kwa wakati na kwani Serikali imeonesha nia ya dhati ya kufungua uchumi wa Bluu.

Awali, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya (TAFICO) Dkt. Eliamini Kasembe, alisema Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kufufua Shirika hili kwani lina manufaa makubwa kwa wananchi na Taifa kwa Ujumla, "Nia hii thabiti inaweza kufikia malengo ya uanzishwaji wa Shirika hili ikiwa ni pamoja na kutoa Ajira na kuchangia katika kuinua uchumi wa Taifa hili." Alibainisha

.




# Shilingi bilioni 25 zatengwa mapambano dhidi ya UKIMWI.

Serikali kupitia tume ya kudhibiti UKIMWI, TACAIDS imeongeza bajeti ya mapambano dhidi ya UKIMWI kutoka shilingi bilioni 14 katika mwaka wa fedha ulioisha hadi bilioni 25 katika mwaka mpya wa fedha 2023/2024 ili watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI waweze kupata dawa kwa uhakika na kuendeleza shughuli zao.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri Ofisi Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Ummy Nderiananga, alipowatembelea watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI katika Halmashauri ya Mji wa Njombe ambapo alisema lengo la Serikali ni kuona WAVIU wanaendelea vyema na maisha yao huku wito ukitolewa kwa wanaume

kujiunga kwenye vikundi pindi wanapobainika kuwa na maambukizi. Pia alipongeza hatua ya uanzishwaji wa Konga katika kila Kata akisema hatua hiyo huwaleta pamoja kw akushirikiana katika shughuli za uzalishaji na kujiona ni sehemu ya nguvu kazi ya Taifa.

"Niupongeze Mkoa wa Njombe mmepiga hatua kubwa sana katika mapambano dhidi ya UKIMWI,kuanzishwa kwa Konga hizi katika kila Kata inaleta faraja kwa WAVIU kwani wanapata fursa ya kujadili mambo yao na kufanyiwa kazi ,"Alisema Mhe. Ummy.

Vilevile Mhe. Ummy alibainisha kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan imejidhatiti kuhakikisha wananchi wake wanaimarika kiuchumi hivyo akawahimiza WAVIU kujitokeza kwa wingi kuchukua mikopo ili kuboresha shughuli zao. Katika hatua nyingine aliwahimiza wanaume kujitokeza kwa wingi kupima afya zao na kujitambua mapema hali zao na kuanza mara moja matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI

"Kwa mujibu wa takwimu inaonyesha watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa Mkoa wa Njombe ni zaidi ya 63,000 huku wanaume takribani 31,372 kwa Mkoa mzima wamepima afya zao nitumie nafasi hii kupongeza konga zetu na wadau wa maendeleo wakiwemo NACOPHA pamoja na hamasa kubwa iliyotolewa na Mhe. Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,"Alibainisha.

Aidha aliwasisitiza kutosita kujitokeza kuchukua mkopo wa asilimia 10 ambao hutolewa na Serikali kupitia Halmashauri pindi mfumo huo wa mikopo utakaporejeshwa tena.

Naye Mratibu wa UKIMWI Halmashauri ya Mji wa Njombe Bwa. Daniel Mwasongwe alisema Halmashauri hiyo imefanikiwa kuwafikia wateja wapya 12,717 katika huduma ya upimaji kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi mwaka huu na kuwaunganisha na Huduma ya Dawa kwa waliokutwa na VVU.



# NAIBU WAZIRI NDERIANANGA Akemea unyanyapaa kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI -WAVIU Nchini

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Mhe.Ummy Nderiananga amekemea vitendo vya unyanyapaa kwa watu wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (WAVIU) na kuiasa jamii kuendelea kuwajali na kuwajumuisha katika shughuli mbalimbali za kujiletea maendeleo.

Ametoa kauli hiyo wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa shughuli za WAVIU, katika Konga za watu wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI katika Wilaya za Moshi ambapo alifanikiwa kuzungumza nao na kukagua shughuli za uzalishaji wanazofanya.

Mhe. Ummy aliitaka jamii kutowanyanyapaa watu wanaoishi na VVU na kuwashirikisha katika shughuli za kijamii na za uzalishaji mali, huku akieleza kuwa ni watu muhimu na wenye mchango chanya kwenye kujiletea maendeleo yao na Taifa.

"Tuache unyanyapaa kwa WAVIU, tusiwabague, tuishi nao kama watu wengine, tuwapende na tujenge tabia ya kuwathamini, kujali na kuwajumuisha katika masuala mbalimbali ya uzalishaji huku tukiunga mkono jitihada za Serikali za kupinga unyanyapaa huo," alisema Mhe. Nderiananga

Aidha alitumia fursa hiyo kuwakumbusha vijana wanaoishi na maambukizi ya VVU kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na Halmashauri zao kujiongezea mitaji na kujikwamua kiuchumi kwa kuwa na vikundi vya uzalishaji mali huku akiwakumbusha kuendelea kujali afya zao kwa kutumia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI.

"Kwa tunaoendelea kutumia dawa za ARVs niwasihii sana tusiache wala kuzipuuza, tumeona zinasaidia wengi na nitoe rai kwa kila anayegundulika na maambuki ya Virusi vya UKIMWI, basi ni vyema aanze dawa hizi mapema ili aweze kuishi katika hali bora zaidi," alisisitiza

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu alitumia nafasi yake kukumbusha vijana kujitokeza kwa wingi kupima na kujua hali zao huku akiwakumbusha kuwa ndilo kundi linaloathiriwa zaidi na maambukizi ya VVU na UKIMWI.

"Pamoja na jitihada za Serikali katika mapambano haya, bado vijana mnakazi kubwa ya kuendelea kujilinda kwa njia zote muhimu zinazoshauriwa na wataalam wa afya huku mkikumbuka kuachana na tabia zote hatarishi zinazoweza kuchochea mtu kupata maambukizi haya," alieleza Mhe. Babu.

Awali akitoa taarifa fupi ya hali ya UKIMWI kwa Mkoa wa Kilimanjaro, mratibu wa masuala ya UKIMWI Mtambuka Bi. Jesca Nyaki alisema kiwango cha maambukizi kimeendelea kupungua kwa kuzingatia takwimu zilizopo, ambapo kimepungua kutoka asilimia 7.3 kwa mwaka 2003/24 hadi asilimia 2.6 mwaka 2016/17.